TANGAZO LA SERIKALI NA. 446 la tarehe 7/6/2024

SHERIA YA MISITU
(SURA YA 323)

# AMRI

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 29(1))*

AMRI YA KUTANGAZA MABADILIKO YA MPAKA WA MSITU WA HIFADHI WEST CHENENE YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kutangaza Mabadiliko ya Mpaka wa Msitu wa Hifadhi West Chenene ya Mwaka 2024.

Tangazo

Ts. Na. 282 la 1989

2. Eneo la ardhi ndani ya mipaka iliyoainishwa katika Tangazo la Msitu wa Hifadhi West Chenene linafanyiwa mabadiliko kusomeka na kuonekana kama lilivyochorwa katika Ramani iliyoainishwa katika Jedwali la Amri hii.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

WILAYA ZA BAHI, CHAMWINO NA CHEMBA

MSITU WA HIFADHI WA WEST CHENENE

*Makadirio ya eneo:* Hekta 27649.77 au Kilometa za Mraba 276.49

Unakopatikana na Mipaka

Eneo lote la hifadhi awali chini ya Msitu wa Hifadhi wa West Chenene linalopatikana Wilaya za Bahi, Chamwino na Chemba, Mkoa wa Dodoma kama lilivyochorwa katika Ramani ya Idara ya Upimaji Jb 2709 ya mwaka 2016 (Skeli 1:50,000) iliyohifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Idara ya Upimaji na Ramani ya Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, na lenye mipaka ifuatayo:

*Tangazo La Serikali Na. 446 (Linaendelea)*




Dodoma,<br>
__24 Mei, 2024

ANGELLAH JASMINE KAIRUKI<br>
*Waziri wa Maliasili na Utalii*